JUNE MMXXIV-TOLEO LA XXXIII

# NGURUMO

*ya mwandishi*



FRANK BROWN MASAI

# KISWAHILI cha MSWAHILI...

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Kiswahili cha Mswahili —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— HAMIDU MCHAKO — Uk 03

**New In Town:** MUUAJI WA MWAKA MPYA na NGUVU YA KIAPO **—** uk 04

**PITIO LA VITABU**— DIWANI YA KIMBUNGA '5'—Uk 06

**MAKALA— SAIKOLOJIA**: Itunze Nguvu Yako ya Asili —Uk 06 na 07

**MAKALA:** Zi' Wapi Kalamu Hizi?**—**uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '08'— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Martin Mazungwa **—**Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '4'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '15'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '12'- Uk 16

**HABARI:** Mtoto wa Afrika Yafana 'Argentina' – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** RAFU ya Fadhy Mtanga —Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** Core Genius —Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO:** Tuwapende Tuwalinde **—** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '2'-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Ukamataji, aupekuzi na Dhamana ya Polisi '4' — Uk 24 na 25

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

# TAHARIRI:
# KISWAHILI cha MSWAHILI

Wasalaam!

Tumeumaliza mwezi wa sita na sasa tu' mwezi wa saba, katikati kabisa ya mwaka huu wa 2024 kadiri ya kalenda zetu. Mwezi wa saba ndiyo ule ambao tangu utoto wetu tumekuwa na shauku sana ya kufika kuona maonesho ya biashara, maarufu kama Saba Saba. Pale tulicheza, tulikula, tulifurahi sana.

Sitaki kuzungumzia hilo, bali lile ambalo miaka miwili iliyopita tulianza uliazimisha kiulimwengu mara baada ya UNESCO kuitaja rasmi tarehe saba ya mwezi wa saba kila mwaka kuwa ni siku maalum ya 'Kiswahili Duniani'.

Ndiyo! Ni Siku ya Kiswahili Duniani. Hapa kwetu tukafupisha na kuiita MASIKIDU, yaani MAazimisho ya SIku ya Kiswahili Duniani. Katika miaka hii ya karibuni, kila kona duniani Kiswahili chatukuzwa. Hii ni lugha kutoka ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki. Lugha rasmi ya mawasiliano hapa Tanzania. Lakini pia sasa, Umoja wa Afrika umeiteua kuwa ni lugha ya kutumia kwenye vikao vyake. Kwa mtazamo wangu mimi hii ndiyo lugha ya Afrika, kwa Waafrika. Kwanini Afrika tusijivune nayo?

Kwa mtazamo wangu, kama Afrika tukiamua na kufanikisha Kiswahili kuwa lugha rasmi na ifundishwe na kutumika barani kote, itakuwa ni hatua kubwa sana ya maendeleo kwa bara letu kwa sababu tutakuwa tunajitoa kwenye makucha ya mkoloni anayetuaminisha kuwa lugha yake ndiyo bora sana. Kutumia lugha ya mtu mwingine na kuamini ndiyo yako, ni kutawaliwa na mwenye lugha hiyo. Tujitambue!

Tukiweza kufikia kipindi cha mtu kutoka nje ya Afrika ili aweze kuwasiliana na Waafrika ni lazima ajifunze Kiswahili, tutakuwa tayari tumeanza kuitawala dunia. Maana wote watakuwa wetu!

Kwani hatuwezi? Tunaweza na tumeshaanza. Lakini katika hili kuna jambo la kushangaza kidogo ila ni la hatari sana kwetu Waswahili. Waswahili hatujulikani kama sisi ndiyo wenye Kiswahili huko *Ughaibuni.* Kwanini? Kwa sababu; kwanza, sisi wenyewe Waswahili hatukipi uzito Kiswahili, tunabanangabananga tu maneno. Tunaamini nikiongea Kiingereza au Kifaransa basi nitaonekana msomi. Wewe! Nani aliyekwambia kuwa kujua lugha ya kigeni ndiyo usomi?

Tujifunze na tuithamini lugha yetu. Huu ndiyo utambulisho popote tutakapokwenda. Jivunie, ongea, tangaza Kiswahili. Yatupasa kuwa Waswahili kwenye kila kitu. Ili mwisho ulimwengu ujue kuwa 'Kiswahili cha Mswahili.'

***Richard Mwambe!***
***WhatsApp 0766974865***

# MWANDISHI WETU: HAMIDU MCHAKO

**Hamidu Mchako aliwahi kuchapishwa katika toleo letu la 11 lililotoka mwezi Agosti, 2022. Ni kipindi kirefu, hivyo basi katika toleo letu la 33 tumeona si vibaya tukimrudisha hapa safuni.**

**Kwa wale wasomaji wapya watapata nafasi ya kumjua na kumsoma mtunzi huyu wa zama hizi. Zaidi ya hapo waweza wasiliana naye pia. Hamidu anajieleza juu ya safari yake ya uandishi...**

Nilipata Elimu yangu ya msingi katika shule ya TAULA Iliyopo Tanga wilaya ya Handeni. Nilifaulu kwenda shule ya upili ya KWEDIZINGA hadi nikahitimu kidato cha Nne.
Sikufanikiwa kuendelea kidato cha tano bali nilipata nafasi ya kwenda chuo cha uuguzi na nikachukua mafunzo hayo. Nilifaulu, na kwa sasa ukiachana na kazi ya uandishi ninauza dawa katika duka la dawa muhimu.

Nina umri wa miaka 26. Pia Nipo kwenye ndoa yenye watoto wawili; wa kike na kiume. Ndoto zangu Ni kufika mbali katika kazi zangu zote hasa kazi ya sanaa nina ndoto ya kuwa mtunzi mkubwa nchini na pia kuandika vitabu vya hadithi zangu na kuzicheza filamu pia.
Nilitambua kipaji changu nilipokua darasa la tatu. Sikuwa mpenzi wa kusikiliza hadithi zilipokua zikisimuliwa nyumbani. Siku moja nikiwa darasani mwalimu wa somo la Kiswahili alipoingia alitaka tusimulie hadithi na kwa msisitizo alisema.

*"Nitateua mmoja mmoja asimulie hadithi na atakaeshindwa atapata viboko vitatu"*
Aliteua baadhi ya wanafunzi na ikafika zamu yangu.
Sikuwa na hadithi yoyote kichwani. Kwa woga wa kupigwa viboko ilibidi hapo hapo nitunge hadithi huku naisimulia.

Na nilitunga na kusimulia hadithi nzuri tena yenye funzo zuri na nilipoulizwa inatufunza nini pia nilijibu. Nilipigiwa makofi na hapo ndipo nikatambua kipaji changu.

Haikuwa kazi ndogo kukikuza kipaji changu hivyo nilizidi kujifunza na kusoma sana hadithi za watu walio na weledi na uandishi mzuri ili nipate njia bora za uandishi.
Nilipozifahamu niliendelea kuandika sasa hadithi zangu.
Sikuwa na simu janja wala computer mpakato.
Hivyo ilinilazimu niandike kwenye daftari kubwa *(Caunter Book).*
Ilipofika mwaka 2007 nilipata simu ya kawaida hapo nilifungua Account ya Facebook.
Nikakutana na waandishi wengi waliofanya nizidi kuimarika.
Ulipofika mwaka 2009 nilipata simu janja nikaanzisha ukurasa Facebook uitwao.

Simulizi kali za Hamidu Mchako
Nilianza kutuma hadithi zangu humo.
Hadithi yangu ya kwanza iliyonipa jina na umaarufu na kupendwa na zaidi ya watu 10000 ilikua ni. MZIMU UMERUDI TENA.

Hadi sasa Nina kurasa yangu inawatu Elfu kumi na mbili na ina hadithi zifuatazo.
1. MZIMU UMERUDI TENA EPISODE 01-103 FINAL
2. KIFO NDIO HUKUMU YANGU
3. KWANINI NIKO JELA
4. KISASI CHA DOCTOR 1-8 FINAL
5. SABABU NI WEWE MKE WANGU
6. NAJUTA KUKUSALITI
7. MLINZI MONCHWARI



8. BABA UMEMUUA MAMA*

Kwa mwenye kuzihitaji atatumiwa kwa njia ya WhatsApp.
Kwa yeyote anayetaka kufanya kazi na mimi kama kuzicheza filamu au kumpa wazo la hadithi .

Mawasiliano yangu

WhatsApp: 0686368823
Call or sms: 0686368823
Email: hamidumchako7@gmail.com

Facebook: HAMIDU MCHAKO
YOUTUBE CHANEL: Simulizi kali za hamidu mchako.

# NEW IN TOWN :
## MUUAJI WA MWAKA MPYA na NGUVU YA KIAPO

**NGUVU YA KIAPO — Na Eva Mrema**

Mwanamama Tabita Komba, kwa unyoofu wa moyo, aliridhia kukifunua kitabu cha maisha yake ya penzi la dhati, lililoishi hata baada ya *omega* kutangazwa.

Kwa wengine, neno 'omega' humaanisha tamati. Kwa Tabita, mambo yalikuwa tofauti kabisa. Jambo moja lisiloaminika, yeye alilikingia kifua na kulisema mara nyingi kwa ujasiri.

"UNATANGULIA MWENDO KABLA YA KUJA KILEMA"

Kurasa ya kwanza ni kama utani wa kirafiki, uliogeuka haraka kama kimbunga na kuwa penzi lenye kila sifa ya kuitwa la dhati. Katikati ya furaha ya habari njema ya ujio wa mtoto, jambo baya linatokea. Ajali mbaya inayombadilisha Tabita jina na kuitwa mlemavu. Haikuugusa hata chembe moyo uliyojaa mapenzi wa Sunche Godwill.

"Karibu mtori, nyama ziko chini"

Kitabu hiki Nguvu ya KIAPO kipo madukani sasa.

Wasiliana na Mwandishi Eva Mrema kwa
**Simu: 0742630141**
**WhatsApp: 0742630141**

Au fika
**Posta Mpya kwa George**
**Bei ni Tsh 12,000**




**MUUAJI WA MWAKA WA MWAKA MPYA - Hussein Issa Tuwa**

Kila mkesha wa mwaka mpya kwa miaka miwili mtawalia, polisi wanaokota maiti huku kando yake kukiwa kuna barua maalum kwenda kwa IGP. Safari hii IGP anaazimia kumnasa muuaji huyo kabla hajaua tena. Je ataweza kuukawiza mwaka mpya usiingie?

Vifo vya kikatili kwa wanadada wapenda mazoezi vinamfanya muuaji mwingine apewe jina "mwiba" - mpaka pale anapotokea mjanja wa mtandaoni na kumbeza muuaji huyo kuwa si lolote, si chochote mbele yake; na kwamba huo mwiba wake ni butu na unahitaji kuchongwa. Je mwiba nao huchongwa?

Wizi wa mamilioni uliopangwa vyema unatimia bila mwenye mali kung'amua, wala mwizi kunufaika. Kivipi?

Na mwingine mkware mwenye sauti ya kushangaza anaingia kwenye chumba cha usaili wa maombi ya kazi, lakini mbona maswali anayoulizwa yanamhusu yeye binafsi badala ya ile kazi aliyoomba?

Mume aliyekosa uaminifu kwenye ndoa aulilia msamaha wa mkewe na kuahidi kuacha kabisa ile tabia yake chafu… na siku anapopewa msamaha huo ndipo anapoamua kumpa talaka mkewe. Ni kwamba kuna kemikali baina yao ama...?


KITABU: MUUAJI WA MWAKA MPYA kipo sokoni kwa Tsh 15,000 tu. Fika duka la Kona ya Riwaya Kinondoni…

**Simu: 0655428085**
**Whatsapp: 0655428085**

- **Posta Mpya—kwa George**


**Simu 0755454152**

- **Elite Tangi Bovu**
- **Kalamu Tulivu Magomeni**



# KITABU: KIMBUNGA (DIWANI) - 4






Katika shairi la "Usimpige Mkeo " mwandishi anasema kuwa haifai mwanaume kumpiga mke wake na vile vile mwanaume hatakiwi kumwekea mkewe masharti magumu.

Shairi la "Hongera" mwandishi anawaonya wanandoa (bibi na bwana) wasiwe na tabia ya kufukuzana wawapo nyumbani. Amewapa kila mmoja maadili yake kwa mwenzake. Beti za (4-5) mwandishi anasema:-

4-*"Bi arusi yangu shika, uyatie akilini.*

*Muumeo akifika, anapotoka kazini,*

*Mpe mema mamlaka, aliwazike moyo,*

*Hongera!*

5- *"Bwana arusi sikia, ukiwa kwako nyumbani,*

*Maneno ya kutupia,hayafai asilani,*

*Kauli njema tumia, na lugha iwe laini,*

*Hongera"*

Katika shairi la "Sifa ya Mke" msanii anaonesha kuwa sifa kubwa ya mwanamke ni tabia na wala si sura. Sifa ya tabia njema humpa mwanamke taadhima, huruma, utiifu na hata uhodari. Anaeleza kuwa mwanamke anapaswa kuwa mtulivu, asiwe kiruka njia, asiwe na ufedhuli wa aina yoyote, uovu, n.k.

Katika shairi la "Sitaki" mwandishi anakemea mapenzi ya udanganyifu yaliyoshamiri katika jamii zetu kwa wakati huu. Mwandishi anasema:-

*"Rabi sinipe mapenzi, hakuna wa kuamini,*

*Wapendwa wenye ujuzi, ni wachache duniani,*

*Penzi la siku hizi, kuhadaana nyoyoni,*

*Mapenzi yamepotea, sasa ni adimu sana,"*

Ni kweli mapenzi ya siku hizi hutawaliwa na pesa na yamejaa ulaghai wa kila aina pamoja na udanganyifu.Mwandishi anaitaka jamii kutambua kuwa mapenzi ya pesa si mapenzi ya kweli hivyo ni vyema yapigwe vita.

**8. Maonyo na maadili mema katika maisha**

Mwandishi amekuwa mwalimu mzuri wa walimwengu kuhusiana na harakati mbali mbali za maisha.Mawaidha aliyoyatoa mwandishi ni kielelezo kizuri kinachofaa kufuatwa na kizazi hiki.Maadili na maonyo haya ni ya muhimu sana katika maisha.Maadili hayo ni kama vile:-

(a)Malezi bora katika jamii ni njia pekee ya kuiweka jamii katika msingi bora wa maisha.Katika shairi la *"Vijana wa Zanzibar"* Mwandishi ameonesha matendo ambayo vijana wa siku hizi wanayatenda ambayo si mazuri pia ni ya kusikitisha.vijana wa siku hizi hawana utii,ni wajeuri, ni wadanganyifu,ni majambazi na pia hudharau mila na desturi zetu za asili na kukimbilia tamaduni za kigeni.Katika ubeti wa 2 msanii anasema:-

*"Mwawacha yenu ya hapa, ambayo yako mazuri,*

*Kutii na kuogopa, mwaona hakuna kheri,*

*Mwayavamia kwa pupa, kwa kedi na ujeuri,*

*Mila zetu za fakhari, wacheni kuzipotosha."*

Kulingana na ubeti huu mwandishi anaonesha kuwa suala la malezi bora ni muhimu sana katika jamii ili kuwaandaa vijana wetu kuendana na mazingira wanamoishi.

Kwa ujumla, katika suala la malezi mwandishi anaifundisha jamii kuwa,samaki mkunje angali mbichi.

b)Umuhimu wa kuwathamini wazazi

Mwandishi ameonesha kuwa kuna umuhimu wa kuwaheshimu na kuwathamini wazazi.Katika shairi la *"Wazazi"* msanii ameonesha kuwa wazazi ndiyo ngao ya mtoto; hivyo mtoto hatakiwi kuwakasirikia,kuwaudhi wala kuwachikiza bali anatakiwa kuwa na mapenzi nao.Wajibu wa wazazi kwa mtoto ni kumpa chakula, mavazi,malezi mema pamoja na elimu.Katika ubeti wa 4 msanii anasema;

*"Wakatafuta walimu,kukupatia ujuzi,*

*Wakakufunza elimu,pamoja na matumizi,*

*Sasa ni mtu timamu,waendelea na kazi,*

*Usiwaudhi wazazi,hiyo ndiyo yako ngao"*

***Itaendelea...***

# -SAIKOLOJIA-

## ITUNZE NGUVU YA ASILI

**Madam Neema Mbilinyi Mgao**
**Simu: 0746 139 654**
**Whatsapp: 0746 139 654**
**Dodoma.**



### ITUNZE NGUVU YA ASILI

Uhali gani mpenzi msomaji wa jarida hili hasa katika makala hii ya Saikolojia. Nikusihi tu kuwa chochote unachopitia uwe na uhimilivu wa moyo ili kuikabiri changamoto hiyo.

Leo nitazungumzia namna ya kuitunza nguvu yako ya asili.

### NGUVU YA ASILI NI NINI?

Nguvu ya asili ni uwezo mkubwa wa mtu ambao ameumbwa nao na Mungu.
Uwezo wa kuongea hadi kushawishi watu wakakubaliana wewe, hiyo ni nguvu ya asili.
Uwezo wa kusuluhisha watu, hiyo ni nguvu ya asili.

Nguvu ya asili ni talanta ambayo kila mmoja amejaaliwa kwa wakati wake. Matumizi sahihi ya nguvu ya asili huleta matokeo chanya kwa mtu husika. Mfano, mwenye talanta ya usuluhishi akiitumia vizuri hiyo nguvu yake ya asili huweza kurithisha amani kwa wengine.

Nguvu ya asili isipotumika ipasavyo huleta madhara, mathalani, mwenye nguvu akazitumia nguvu zake katika ujambazi na unyang'anyi huweza huleta madhara sio tu kwake binafsi bali hata kwa jamii.

**Faida za nguvu ya asili**

**1. Huleta watu pamoja.**
Nguvu ya asili, ikitumika ipasavyo, huleta watu pamoja. Yawezekana nguvu yako ya asili ipo katika kuwafundisha watu namna nzuri ya kuishi. Muda ule unapofundisha ni wazi kuwa watu watakaa pamoja kukusikiliza. Nguvu hiyo ya asili itakusaidia kuzikusanya akili za wale watu kwa wakati ule na ukazimiliki na kuwaelekeza watu vile inafaa wawe.

**2. Itakufanya kujitawala**
Utakapojitambua kuwa nguvu yako ya asili ipo wapi basi itakufanya kujitawala wewe mwenyewe binafsi, hii ni faida kubwa sana, kwamba uwe na uwezo wa kujitawala na kujiamini wewe mwenyewe. Faida ya nguvu ya asili ni kwamba inakupa kujielewa, kujitambua na kujitawala.

**3. Inakutofautisha na mwingine**
Kama nilivyosema,nguvu ya asili ni muungano wa talanta ya kila mmoja na alivyoumbwa, kumbe nguvu hiyo uliyonayo inakutofautisha na mwingine. Kila mmoja na ujazo wa talanta yake pale mahali Mungu amempendelea kuwa yeye.

**KWANINI MTU HUIPUNGUZA AU KUIPOTEZA KABISA NGUVU YA ASILI.?**
Kama tulivyoona hapo mwanzo, kila mtu ameumbwa kwa uwezo wake binafsi. Ameumbwa na talanta yake halisi ila hufikia wakati ile nguvu ya asili hupotea. Wataalamu wengi wa Saikolojia na hata utafiti nilioufanya na mimi pia, nikajiridhisha kuwa huwa inafikia hatua mtu huupoteza ule uwezo wake asilia aidha kwa kujua au kwa kutokujua. Ghafla tu hushtukia uwezo wake umempungua. Ghafla tu au taratibu mtu huona mbona sasa akizungumza na watu hawamzingatii tena? ghafla tu anaona mbona kama watu hawamtilii maanani tena? Mbona watu hawamkubali tena? Zipo sababu kadhaa ambazo hupelekea hali hiyo, hapa tuone baadhi.

**A. Kujidhalilisha.**
Wataalamu wengi wa maswala ya afya ya akili katika jamii waliliona hili kama sababu ya mtu kupungukiwa nguvu ya asili katika ile jamii imzungukayo, mathalani, pengine ukawa mshauri mzuri wa maswala ya ndoa, lakini kutwa kucha jirani zako wanashuhudia ukipigana na mwenzi wako mpaka kufikia kuvuana nguo, unategemea ile jamii itakuheshimu? Na kadri jamii inavyokuonesha kutokukuheshimu ndivyo na wewe unapoanza kujishusha uwezo wako wa usuluhishi, mwisho wa siku ile hali ya kujiamini na kuiamini nguvu ya asili hupotea.

# -SAIKOLOJIA-
# ITUNZE NGUVU YA ASILI

**2. Kudharauliwa/kubezwa.**
Nguvu ya asili huchochewa na namna unavyokubalika kwa watu, vile wanavyoonesha kukupokea, kama wakikuonesha kukudharau, kukubeza, ni wazi kuwa hata wewe ule moyo wa kufanya unachofanya utapotea, na utajiuliza kwanini uendelee kufanya? na utakapoacha kufanya basi ni wazi kuwa ile nguvu ya asili italala.

**3. Kuwa na mahusiano ( wanaume au wanawake wengi kwa wakati mmoja).**
Hapa tuelewane sawa sawa, na ni maombi yangu kwa Mungu kama nazungumza na mtu alielaza nguvu yake ya asili basi chunguza, pengine hii ni sababu.

Wataalamu wengi sana wamethibitisha kuwa, unapojamiiana(sex), iwe umetumia kinga au la, zipo nguvu za kila mmoja wenu zinaingiliana. Yaani unapofanya mapenzi kama unaefanya nae anamajini basi yanatoka kwake na kuja kwako (naongea kwa lugha rahisi ili unielewe), kwamba kama ni bahati pia zinaingiliana. Kuwa bahati ya huyu inaingia kwa huyu pia. Walienda mbali zaidi wakasema, mtu ni lazima anazo pande mbili, yaani bahati nzuri na mbaya ( mikosi).
Nikafanya uchunguzi na mimi pia, kwa wale walioridhia na wakanipa majibu sahihi, wakathibitisha kuwa, katika mahusiano unaweza kuanzisha mahusiano na mwanamke au na mwanaume huyu, na mambo yako yakawa yanaenda sawia, ukapata bahati ya mambo mengi sana tofauti na kabla ya haujaanzisha na huyo mtu. Au ukaanziasha mahusiano na mtu, ukajikuta siku ya kwanza tu ya mahusiano mara umeanguka sijui mguu umefyatuka,mara kadri mnavyoenda wewe ikawa kila iitwapo leo ni mtu wa matatizo tu (Kama haujawahi kuchunguza, chunguza, halafu unijibu). Wataalamu wanasema 'zipo nguvu za asili kwa kila mmoja ambapo huwa za baraka au za laana, watu wanapojamiiana hubadilishana nguvu hizo'. Kwa tafiti mbalimbali nilizozifanya, nikajiridhisha kuwa,wapo watu waliopoteza nguvu zao za asili kwa njia hii ya kujamiiana hovyo.

**4. Matumizi ya nguvu za kishirikina**
Nazungumza na wale ambao mambo yao hayaendi bila kuoga dawa za waganga. Leo kaenda kwa mganga kiboko kule DRC mara karudi kaenda Sumbawanga, mara aende kwa mganga Tanga, unapoteza nguvu ya asili yako. Utafiti unasema, kila mtu anayo ile nguvu ya asili inayotoka kwa Mungu, na sio kwa mwanadamu. Unapoingiza nguvu za kishirikina unaiua ile nguvu yako ya asili. Ingawa sikatai, wapo watu hulazimika kwenda kwa waganga kutokana na mapito ya ulimwengu lakini amini kuwa kadri unavyozidi kwenda kwa wataalamu basi ndivyo unavyozidi kuua ile nguvu yako ya asili na Mungu wako.

**ITUNZE NGUVU YA ASILI**
Kila mmoja ameumbwa tofauti na mwingine, nguvu yako ya asili ni tofauti na nguvu yangu ya asili. Na inawezekana kabisa kuwa mtu mmoja akawa na nguvu ya asili ya kumfanikishia mambo yake kila iitwapo leo na kwa mkusanyiko wa mambo mengi pia. Pengine akishika biashara inaenda tu, huyo huyo akiajiriwa pia anafanya vizuri sana. Hiyo inawezekana kabisa. Itunze hiyo nguvu yako ya asili, usiichafuechafue hovyo kwa sababu za hapo juu na baadhi ya sababu zinginezo utakazozivumbua.

**Naifufuaje nguvu yangu ya asili?**
Sasa baada ya kusoma hapo juu, pengine unasema sawa Madam Neema, mi ndio nimeshayabananga (nimeshakosea). Kwamba unasema siioni tena nguvu yangu ya asili,nifanyaje?. Vizuri, hapa nakuletea njia halisia zaidi ambazo naziamini na zimeaminika na wataalamu wengi.

**a} Kumuomba Mungu.**
Hii ni njia ya kwanza kabisa na ni njia kubwa kabisa. Fanya ibada kwa Mungu wako. Omba toba kwa Mungu wako, jiweke ndani ya uwepo wa Mungu kwa kuwa karibu na nyumba za ibada kwa imani yako. Kama ni msikitini nenda msikitini, kama ni kanisani nenda kanisani.

**b} Jiamshe upya**
Saikolojia ya akili yako ikikuthibitishia kuwa uwezo wako umepungua basi haraka sana jiamshe upya wewe mwenyewe. Hii inaweza kuwa tiba nzuri sana ukijifanyia. Kwanza tafakari ni wapi au ni kwa sababu zipi za pale juu nilizoziainiasha zimekupelekea kupunguza au kulaza uwezo wako wa asili. Ukishazijua sababu basi anza kuzipangua sababu zote.

***Inaendelea ukurasa wa 25***

# MAKALA: Zi' wapi 'KALAMU' hizi?

Na Richard Mwambe

Baruapepe; jamvilasimulizi@gmail.com/ WhatsApp; 0766974865

KILA mja, Mwenyezi Mungu kamuumba na ulevi wake. Au nitumie neno zuri 'udhaifu'. Mimi, wewe, yule na hata yule kuleee, sote, kila mmoja ana ulevi au udhaifu wake. Ulevi au udhaifu huo, waweza kuwa mbaya au mzuri. Inategemeana.

Kuna watu ni walevi wa pombe. Yaani bila kunywa pombe maisha yao hayaendi. Huu ni ulevi mbaya sana maana unaharibu afya yako ambayo Mungu amekupa. Kwa kunywa pombe, unahatarisha ini, figo na uwezo wa kufikiri kwa ujumla.

Kuna wengine bila sigara, yaani utamuonea huruma. Ina maana sigara ni moja ya kiungo chake cha mwili? Hatari! Ulevi wa sigara uhatarisha afya ya mapafu, mifumo ya upumuaji na hata ubongo.

Halafu kuna walevi wa ngono. Yaani hili ni kundi la watu ambao pasi kupata mwanamke au mwanaume wa *'kungonoka'* naye, maisha kwake hayana thamani kabisa. Lakini anasahau kuwa anahatarisha afya yake ya mwili maana kuna magonjwa mengi kupitia ngono, kama UKIMWI, Kaswende, Pangusa n.k

Kwa ujumla ulevi, ulevi, ulevi. Ulevi ni nini? Ulevi ni kupenda kufanya kitu kupita kiasi iwe kibaya au kizuri. Ukikifanya bila kiasi ni ulevi. Tunda la Roho ni KIASI.

Sasa kuna aina nyingine ya ulevi ambayo wengi ama hawaijui au ni walevi wasiojijua. Huu ni ulevi mzuri wenye matokeo chanya kwa mtu binafsi na hata kwa jamii. Usomaji wa vitabu. Kama usomaji wa vitabu ungekuwa si ulevi, tusingejenga maktaba kubwa kubwa. Maktaba ndiyo 'baa' ya msoma vitabu.

Ingekuwa nina mamlaka ningesema kila baa hapa nchini tuweke vitabu. Kabla hujanywa pombe yako unasoma kwanza kitabu kurasa kadhaa na uandike ulichojifunza. Au kila 'gesti hausi' ungetakiwa kusoma kitabu kwanza wewe na huyo mwenzi wako ndo mpewe chumba. Nina uhakika nchi ingegeuka.

Lakini, ili wasomaji wasome, wanawahitaji waandishi. Je waandishi wa vitabu, mnakidhi mahitaji ya wasomaji? Hapa ndipo nataka tuzungumze.

Usemi wa kwamba 'hakuna wasomaji siku hizi' ufe. Walevi wa vitabu ni wengi sana siku hizi, na wanatafuta maarifa anuai kila kona. Watoto kwa watu wazima. Mwamko huu unapaswa kujibiwa. Na wakutoa jibu hilo ni waandishi. Tanzania tumebarikiwa kuwa na waandishi wengi sana wa vitabu aina aina. Vya hadithi za watoto, watu wazima, majarida, vya ujasiliamali, vya uchumi binafsi, vya kujikomboa kifikra, vya ujana, vya dini n.k. vyote hivi tuna waandishi wazuri wazuri hapa Tanzania kama Joel Nanauka, Denis Mpagaze, Laura Pettie, Hussein Tuwa, Lilian Mbaga, Richard Mabala, Mohamed Hammie, Mzee Beka, Corona Cermak, Magoda Jr na wengine wengi wengi wengi siwezi kutaja wote.

Zipo kalamu ambazo zikiandika basi hukutoa kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Na zipo ambazo zikiandika zitakupa burudani murua kwenye ubongo wako.

Mwandishi na msomaji ni watu wawili wanaokwenda pamoja. Daima tutasema hakuna wasomaji ilihali waandishi hawaandiki. Andika, ukishaandika utamwona msomaji.

Na kinachonisikitisha ni kuwa kuna kalamu haziandiki, sasa sijua zimeisha wino au vipi. Ukimya umepiga kite kwenye uwanda wa fasihi, matokeo yake wanajitokeza wengine na kuandika pasi na misingi ya kiuandishi na kuchafua hali ya hewa ya kifasihi kiasi kwamba hata msomaji anakosa hamu ya kusoma.

Zi' wapi kalamu hizi? Ibrahim Gama, Maundu Mwingizi, Kajubi Mukajanga, Hussein Wamaywa, Innocent Ndayanse, na wengine wengi, wa kale kwa wa zama hizi?

Uandishi wenu bado unatakiwa na unahitajiwa na wasomaji. Kazi zenu zimepungua kama si kutoweka madukani.

Sisi *walevi* wa vitabu tu' hapa twasubiri. Haya shime mtukumbuke…


The Grand Kagera Tour
THE GRAND
KAGERA TOUR
UZUNDUZI WA VIVUTIO VYA UTALII
MICHEZO
SHEREHE ZA KIMILA
UTALII
KITALAMO
IJUMAA
KAGERA - KARAGWE
12 JULY 2024
+255 782 054 720
@thegrand_kagera_tour


SEPENGA ENTERTAINMENTS
12 JULY
20 24
The Grand Kagera-Tour
THE GRAND
KAGERA TOUR
KAGERA
KARAGWE
UZINDUZI WA VIVUTIO VYA UTALII
NI MUDA WA KWENDA KULA SENENE
IJUMAA
10 AM


JAMVI LA SIMULIZI
MOBILE BOOKSHOP
VUKA UJANA SALAMA Inawezekana
FURAHA A KABAGE
VUKA
UJANA
SALAMA
inawezekana
Tupigie/WhatsApp
0766974865
MPESA LIPA NAMBA
5559006
JAMVI LA SIMULIZI
Tsh
10,000
•Tunapatikana Gangilonga, Allamano Centre pembeni mwa Chuo Kikuu Huria - IRINGA


IGP 'Kamari Ya Roho'
Tsh 4000 UPDF
lipa kwa
Mpesa Lipa Namba
5559006
JAMVI LA SIMULIZI
Kamanda Amata
IGP
WhatsApp +255 766 974865



Muamar Muhammad Abu Minyar Al - Gadafi

Inaendelea...

**Kamati za Mapinduzi na kuendeleza usoshalisti: 1978-1980**

Mwezi wa Desemba 1978, Gaddafi alijiuzulu kama Katibu Mkuu wa GPC, akatangaza umakini wake mpya kwenye shughuli za mapinduzi badala ya serikali; hii ilikuwa sehemu ya mkazo wake mpya kwenye kutenganisha miundo ya mapinduzi na serikali. Ingawa hakuwa tena katika nafasi rasmi serikalini, alikubali jina la "Kiongozi wa Mapinduzi" na akaendelea kama kamanda mkuu wa vikosi vya jeshi. Mwanahistoria Dirk Vandewalle alisema kuwa licha ya madai ya Jamahiriya kuwa demokrasia moja kwa moja, Libya ilibaki kuwa "mfumo wa kisiasa wa kufukuza wengine ambao maamuzi yao" yalikuwa "yamezuiwa na kikundi kidogo cha washauri na watu wa karibu" waliozunguka Gaddafi.

Libya iligeukia kuelekea kwenye usoshalisti. Mwezi Machi 1978, serikali ilichapisha mwongozo wa ugawaji wa makazi, ikijaribu kuhakikisha kila mtu mzima anamiliki nyumba yake mwenyewe. Familia nyingi zilipigwa marufuku kumiliki zaidi ya nyumba moja, huku mali za kukodisha zamani zikipokonywa na serikali na kuuzwa kwa wapangaji kwa bei iliyopunguzwa sana.

Mwezi wa Septemba, Gaddafi alitoa wito kwa Kamati za Watu kufuta "utawala wa utumishi wa umma" na "udikteta wa sekta binafsi"; Kamati za Watu zilichukua udhibiti wa makampuni kadhaa ya mamia, kuzigeuza kuwa ushirika wa wafanyakazi unaoendeshwa na wawakilishi walioteuliwa.

Mwezi Machi 1979, GPC ilitangaza kugawanyika kwa serikali na mapinduzi, huku yale ya mwisho yakiongozwa na Kamati za Mapinduzi mpya, ambazo ziliendesha kazi zao pamoja na Kamati za Watu katika shule, vyuo vikuu, vyama vya wafanyakazi, polisi, na jeshi. Zikiongozwa na vijana wengi wenye hamasa ya mapinduzi, Kamati za Mapinduzi zilikuwa zimejikita Tripoli na walikutana Gaddafi kila mwaka.

Makala ya kila wiki, The Green March, ilianza Oktoba 1980, na Kamati za Mapinduzi zilichukua udhibiti wa vyombo vya habari. Walikuwa na jukumu la kuendeleza mapinduzi, kufanya uchunguzi wa kiitikadi, na kuchukua jukumu kubwa la usalama, kukamata watu na kuwafikisha mahakamani kwa mujibu wa "sheria ya mapinduzi".

Bila taratibu za kisheria au kinga, utawala wa haki ya mapinduzi ulikuwa wa kiholela sana na ulisababisha unyanyasaji mkubwa na ukandamizaji wa uhuru wa kiraia: "Green Terror".

*Itaendelea...*



Muammar Gaddafi akiwa kapakata mtoto.

# SAKO KWA BAKO:

## Martin mazungwa—mwamuzi wa soka, msoma vitabu

**Safari yetu ya Ana kwa Ana bado inarandaranda katika viunga vya Jiji la maraha la Daar es salaam. Hah! Nikakutana na mtu mmoja ambaye kiukweli sikufikiri…**

Huyu hapa msikilize…

**Kiongozi hebu jitambulishe kwanza:**

Naitwa Martin Mazugwa.

Jina kwangu siyo geni, hebu tueleze kazi yako kwanza kama hutojali:

Kazi yangu ni muandishi wa habari za michezo katika gazeti la Habari Leo lakini pia ni mwamuzi wa mchezo wa mpira wa miguu wengine hupenda kuita soka, Kandanda, Kabumbu na mengine mengi.

**Waoh! Amazing! Kumbe inawezekana kuwa mwamuzi wa soka na mwandishi wa habari… asee! Huwa unasoma vitabu pia?**
Binafsi ni msomaji wa vitabu japokuwa siwezi kusema sana lakini najitahidi kila ninapopata muda wa ziada baada ya kumaliza shughuli zangu huwa naumalizia kwenye vitabu
Aina ya vitabu ninavyopenda ni hadithi za taharuki, hivi nimekuwa nikivipa kipaumbele japokuwa pia vitabu vya hadithi za mapenzi huwa nasoma lakini sio kwa wingi

**Sasa… kusoma vitabu ulivyosema inakusaidia nini na kazi yako?**
Usomaji wa vitabu unanisaidia katika kujifunza mambo mengi nje ya karia yangu kujifunza wengine wanafanya nini lakini kubwa nimekuwa ni kupanua wigo katika lugha, kupata misamiati mipya ambayo nimekuwa nikiitumia kwenye shughuli zangu za uandishi

Nimekuwa nikijifunza staili mbalimbali za uandishi kutoka kwa wabobevu wa lugha ya Kiswahili walioamua kutumia kalamu kuelimisha, kuburudisha na kuonya jamii kupitia vitabu.

**Ok! Na hii tabia ya kupenda kusoma vitabu umeipata wapi?**
Tabia ya kusoma nimeifuata kwa baba yangu mzazi yeye alikuwa na kawaida ya kununua vitabu kadiri alivyoweza japokuwa hakutulazimisha kupenda anachopenda, mimi nilivutiwa na utamaduni ule na kuuendeleza hadi hii leo nikiwa na maisha yangu

**Kuna faida?**
Faida ni nyingi sana za usomaji wa vitabu naweza nikazitaja chache; kwanza inanipa nafasi ya kujua mambo mapya kutoka kwa waandishi, pili nimekuwa nikiburudika kwa kusoma riwaya za mapenzi lakini pia kupata mawazo mapya na mbinu mpya hasa kwenye kujenga wahusika

**Hebu tuambie mwaka uliopita umesoma kiasi gani?**
Mwaka 2022 haukuwa mzuri sababu nilisoma vitabu 30 pekee hii ilichangiwa na muda mwingi kutingwa na majukumu ya kiofisi panapo majaaliwa mwaka 2023 huenda nikaongeza idadi ya vitabu vingi zaidi.

**Aaaah 30 si haba hata mimi sijafikisha hiyo mwaka 2022. wito wako ni upi kwa watanzania?**
Wito wangu kwa wazazi wa kitanzania naomba tuwajengee watoto utamaduni wa kujisomea vitabu na kupunguza matumizi ya simu na michezo isiyokuwa na ulazima kwani itawajengea tabia ya udadisi pamoja na kuwapa maarifa mapya ambayo yatawasaidia katika maisha yao.

**Huyu bwana hapendi kuongea sana, hata mimi nikaona nisimchoshe.**
**Bwana Martini Mazungwa, Ngurumo ya Mwandishi inakutakia yote mema katika mwaka huu.**
**Richard Mwambe**



# SHAJARA YA MUUAJI—4

Na. Richard Mwambe



**Aliniwasha makofi humu ndani, hakuelewa lolote ninalomwambia. Likapita, mapenzi yakaendelea... Mimi nilimpigia yule bwana wa car wash... Nikamwambia kilichotokea; hasisikitike, akafurahi akasema atahakikisha tunaachana ili anichukue, na alisema atafanya kila awezalo..."**

***Endelea...***

"Pole!"
"Asante," akajibu Amina akifuta machozi yaliyomtiririka mashavuni mwake. "Siku kama saba nyuma hivi tulikuwa pale Embalele Great Pub, kwenye kona pale, Sikinde walikuwa wanapiga... Yule bwana wa car wash akaja akaniona... Nipo na Sume wangu hapo! Hasione haya! Kaja kanikumbatia kanibusu mdomoni... Kile kitendo sikukitegemea kwa kweli... Sume aliamka, alipiga yule jamaa na mziki ulizimwa... Alimng'oa meno mawili palepale... Tangu hapo sikumsikia yule jamaa..." Sajini Steven akabaki akimtizama Amina. Yule mwanamke akainuka na kwenda kujifungia chumbani kwa dakika kama tano hivi, kisha akarudi.

"Huyo bwana anaitwa nani?"
"Huwezi kuamini, sijawahi kujua jina lake!" Amina akajibu. Sajini Steven akaomba namba yake, akapewa.
"Asante kwa ushirikiano wako. Jeshi la polisi litahakikisha muuaji wa mpenzi wako anatiwa atihani!"
"Nitashukuru... Yaani nitakupa zawadi kubwa sana! Na mkimkamata niambie... Japo makofi mawili nimtandike yatamtosha!" Wakaagana na kubadilishana namba za simu.
Afande Steven alirudi ofisini. Kituo chake cha kazi kilikuwa ni Chang'ombe. Akawasili na kuingia moja kwa moja ofini kwake na kujibwaga kitini. Maelezo machache aliyoyapata kutoka kwa yule mwanamke akayaandika na kuyahifadhi kwenye jalada lililofunguliwa dhidi ya mauaji ya Sume Msamange. Steven hakupenda kumleta Amina kituoni, alijipanga kwenda kumhoji hukohuko aliko, alifanikiwa.

Kabla hajarejea Chang'ombe polisi, aliendesha gari lake mpaka kituo kile cha kuoshea magari.
Akaliingiza na kuliegesha mahali ili lipate huduma.
"Karibu *bro*!" Akakaribishwa na kijana aliyekuwa tayari kulipokea gari lile.
"Asante sana," akamjibu na kumkabidhi funguo huku yeye akifuata maelekezo aliyopewa ya kuingia kwenye ofisi ndogo kwa ajili ya kuandikisha gari hilo. Ndani ya ile ofisi alimkuta mtu mmoja ambaye bila shaka ndiye aliyekuwa mmiliki wa *car wash* ile. Alimtambua haraka kwa sababu kuu mbili; wajihi wake ulishahabiana kabisa na maelezo aliyopewa na Amina, kila alipocheka pengo lake la meno ya Mbele lilionekana. *Hili ndilo pengo Sume Alimng'oa meno!* Akawaza.
Baada ya gari lake kupata huduma stahiki, Steven aliondoka. Ndipo akarudi ofisini.
Mbele, juu ya meza yake palikuwa na kabrasha moja; wao hupenda kuita jalada lenye taarifa za awali za mauaji ya Sume Msamange. Kila alichokipata alikiandika na kukihifadhi humo. Mpaka dakika hiyo alikwishampata mtuhumiwa namba moja ambaye kwake alikuwa ni Jackson Balinga, mmiliki wa Balinga Car Wash. Steven hakuwa na jambo jingine zaidi ya kutoa RB ya kukamatwa bwana huyo. Vijana wa kazi wakaondoka na Defender la polisi kuelekea kule walikoelekezwa.

Saa moja baadae, macho ya Steven yalikuwa ana kwa ana na yale ya Balinga. Walitazamana kama majogoo yapiganayo. Jackson Balinga alifikishwa kituoni hapo saa Tisa alasiri kwa mahojiano.
"Jackson Balinga! Umeletwa hapa ili kulisaidia jeshi la polisi kuthibitisha tuhuma za kuua..." Steven akamwambia.
"Nimemuua nani?"
"Sume Msamange! Jeshi la polisi linakutaka kuandika maelezo yako ya mauaji hayo!" Steven akamwambia na kumsogezea kalamu na karatasi.
"Kha! Mimi sijaua jamani... Mnanionea..." Jackson alilalama.
"Kwani sisi tumesema umeua? Tumesema unatuhumiwa... Sasa ni wajibu wako kuthibitisha kuwa si wewe, japo hilo utalisemea mahakamani. Basi kama hutaki kuandika jibu maswali yafuatayo..." Jackson Balinga akabaki kimya hakujibu lolote kati ya yale aliyoambiwa.
"Unamfahamu Sume Msamange?" Akamuuliza.
"Simjui mimi... Siwezi kujuana na watu wajingawajinga mi nipo mjini kutafuta pesa..." Jackson akajibu huku akiwa amefura kwa hasira.
"Una mahusiano gani na Bi Amina Blengelo?" Swali lile lilimgutusha Jackson.
"Amina?" Akauliza.
"Ndiyo... Amina Blengelo," Steven akaendelea kumweleza.
"Simjui... Nshakwambia mi natafuta

hela mjini hapa," Jackson akajibu kijeuri.
"Pesa zako zisikufanye uwe jeuri sawa dogo?" Steven  aliongea, sasa kwa sauti ya upole iliyojaa maana kubwa. Jackson akashusha pumzi, akaelewa mini maana ya sauti ile.
"Haya, nawajua wote, wote hao mi nawajua. Amina ni demu wa Sume... Haya swali jingine mi niondoke..." Jackson akang'aka.
"Unajua kwamba Sume Msamange ameuawa?"
"Ndiyo najua!"
"Unajuaje?"
"Magazeti yote yameandika na redio zimetangaza kifo chake... Hakuna asiyejua hilo..." Jackson akajibu kwa hasira. Steven , mpelelezi aliyekabidhiwa kesi hiyo akabaki kimya kumwangalia kijana Huyo mwenye mwili uliyonawiri kwa fedha huku akigongagonga meza kwa vidole vyake.

"Unaweza kutuambia kuwa mara ya mwisho ulikutana na Sume wapi?"
"Baa..."
"Halafu nini kikatokea?" Steven akauliza.
"Akanipiga sana..."
"Kwa kuwa ulikuwa unamtaka mpenzi wake siyo? Uliingilia mahusiano yake ni sawa...?"
"Sasa hayo yanaingiaje afande..." Jackson akaongea kwa mshangao.
"Ok, andika yote hayo kwenye hiyo karatasi kisha uondoke zako!" Steven  akamwambia. Sume akavuta lile karatasi na kalamu akaandika kila anachojua. Alipomaliza, Steven  akachukua ile karatasi na kuisoma, kisha akaitia kwenye lile jalada. Akapewa nyingine.
"Hii ya nini sasa?" Akauliza Jackson.
"Andika tena, ile imefutika. Andika vilevile..." Jaksoni alichukia lakini hakuwa na la kusema. Akaandika akamaliza. Steven  akachukua ile karatasi na kuiweka kwenye lile kabrasha. "Afande! Mchukueni huyu mumpatie pa kulala..." Jackson Balinga hakuamini kabisa anachosikia, "unasema?" Akauliza.
"Hivyo ulivyosikia ndivyo," akajibiwa. Jackson pamoja na ujeuri wake wote na pesa zake, akawekwa *lockup*.

Usiku uleule, Amina naye alifikishwa kituoni. Mbinu aliyotumia Steven kqenda kumhoji nyumbani kwake ilikuwa ni kutaka tu mwanamke hiyo awe mwepesi kusema anachojua. Majengo ya polisi yanatisha bwana. Naye alipofikishwa akatakiwa kuandika maelezo. Akafanya hivyo mara tatu. Akiwa pale anaandika alimwona Afande Steven , yule aliyekwenda kumtembelea asubuhi ya Siku ile nyumbani kwake. Lakini Steven  alimpita kama hamjui, kama hajawahi kumwona. Sanasana alimwachia ujumbe askari wa kike kwamba akimaliza amlundike *lockup* tayari kwa Siku inayofuata.
Washukiwa wa awali wa mauaji ya Bwana Sume Msamange; Bi Amina Blengelo na Jackson Balinga walitiwa Nguvuni tayari kupandishwa mahakamani. Hati ya mashtaka ikaandaliwa.

Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865

## 03

**Kigamboni**
**2012, August 8**
**10:06 jioni**

MATHIAS MERENGO, mwanaume mwenye tambo hasa la kiume. Mwili wake mkubwa, mrefu, ulipendezeshwa na ndevu nyingi, nyeusi zenye afya zilizokaa kwa utulivu kidevuni pake na kuzunguka mashavu yake. Ungemwona tu, ungejua kuwa ni mwanaume mwenye pesa.

Kazi yake hakuna aliyeijua, lakini pesa ya kula na kunywa na kuhonga wanawake wazuri wazuri waliobarikiwa shepu alikuwa nazo. Alizipata wapi? Lilikuwa swali la wengi waliomjua. Alijenga nyumba kubwa, nzuri, na ya kisasa katika eneo la Mjimwema huko pande za Kigamboni, kilomita kadhaa kutoka kivukoni. Hakuwa na mke wala mtoto isipokuwa mfanyakazi wake wa ndani aliyempenda sana. Wengine walisema haoi kwa sababu anatembea na mfanyakazi wake wa ndani, wengine wakasema hana uanaume.
***Itaendelea...***

# RIWAYA: CRONOC 7 (15) – richard MWAMBE

**"Yes!" Carlos alikuwa akitoa maelekezo kwa mwanadada aliyekuwa naye ndani ya gari, wakiwa tayari wanamvizia yule mwanadada mfanyakazi wa mapokezi pale hotelini Vatican Wing. "Nikamlete?" mwanadada aliyekuwa kwenye gari la Carlos akauliza.**

***Endelea...***

"Nimepata wazo, ngoja tumfatilie ili tujue anaishi wapi, na hapo tutambania chumbani kwake," Carlos akatoa maelekezo na kuwasha gari.
"Aiyaaaaaa," akajikuta akipiga kelele kwa sauti ya chini.
"Vipi wewe?" jirani yake akauliza.
"Amepanda mabasi ya mwendo kasi…, ok, sasa we nenda kapande lile basi mi nakuja kwa gari, popote atakaposhuka nipe taarifa, na wewe shuka naye," akampa maelekezo na yule mwanadada akateremka na kupanda lile basi jipya kabisa ambalo ni moja ya huduma za usafiri zilizoanza nchini hasa Jiji la Dar es salaam.

Taratibu lile basi liliondoka huku na mengine yakiingia na kutoka. Carlos aliingiza gari barabarni na kulifuata basi hilo kwa pembeni maana ilikatazwa kabisa kupita katika barabara hizo kwa magari ya kawaida. Hivyo alilifuata kwa kutumia barabara ya pembeni akiangalia kwa makini kila kituo ambapo linasimama. Waliiacha barabara ya Msimbazi na kuchukua ile ya Morogoro kuelekea Ubungo.

❦

Madam S bado alikuwa ofisini, akiwa ametingwa katika kusoma kile kitini kilicholetwa na Amata. Ghafla, akagutushwa na mlango uliokuwa ukifunguliwa, na sekunde chache alimwona Chiba akiingia ndani ya ofisi hiyo.

"Karibu!" akamkaribisha huku akikifunga kile kitini.

"Naona unaperuzi…"

"Ndiyo kazi zetu. Chiba nimekupigia simu nataka nikupe kazi kidogo, sawa? Soma hapa kwanza," akamwonesha kile kitini pale juu.

"Cronoc 7, S.S" akatamka kwa sauti.

"Unaweza kuling'amua hili neno ukaelewa maana yake?" Madam akauliza.

"Hebu nipe kwa kifupi tu nini umesoma humo ndani na 'mi naweza kukudadavulia," akasema na Madam S akaanza kumwambia kwa uchache yale yaliyomo humo ndani. Alipomaliza, Chiba akatulia na kutabasamu.


"Siwezi kujua Cronoc 7, ila S.S kwa maelezo uliyonipa itakuwa ni Secret Society, na kama wanaounda sio saba basi hao saba watakuwa ndiyo 'madigala', ila Cronoc inabidi kulifanyia kazi, labda ni hivyo…"

"Shiiiiit!!! Yaani muda wote naumiza kichwa kumbe jibu liko hapa, Secret Society, ok sawa, nimekupata kijana wangu," Madam S akajikuta akiongea kwa furaha.

"Haya na kazi uliyoniitia…"

"Aaaa ok, ya kwanza ndiyo hii umenisaidia kwa asilimia karibia themanini na ya pili ni hii," akampa karatasi yenye majina manne, yale ambayo yapo kwenye kile kitini na yameandikwa chini ya ile aya ya onyo.

Mr. Donald Stephenson – Australia.
Aquald Berret – Mauritius.
Didiof Mathis - Nigeria
Bi Suzan Oromouf – Rusia.
Chiba alipoamaliza kuwasoma akamtazama Madam S.




"Kaniletee data zote za hao watu, kabla ya jua kuchomoza, nina maana kuwa utakapomaliza tu kupata tafutishi zako nipigie simu tuonane hata kama ni saa nane za usiku. Sijaolewa mimi hivyo usiogope," Madam S akatoa oda ya kikazi.

"Copy!" Chiba akajibu na kunyanyuka, akamwacha Madam S ofisini humo peke yake kama alivyomkuta.

❦

Akili ya Kamanda Amata daima ilikuwa ikifanya kazi kuliko kawaida, hii ndiyo hisia ya sita ambayo mwanausalama yeyote, hasa vitengo maalumu huwa nayo na daima hutumiwa kama kigezo kikubwa kwa kupata kazi hiyo. Mara alipoondoka kwa Madam S alijua wazi kuwa yule mwanadada wa mapokezi kule Kurasini atakuwa matatizoni. Hivyo aliendа kuhakikisha anamtazama kama yupo salama au vipi. Akalitoa gari lake barabarani na kuegesha karibu na duka moja la vinywaji. Kutoka pale alipo aliweza

kuliona lile basi likiingia kituoni na kusimama. Tangu Kurasini alikuwa akimfuatilia yule mwanadada aliyempa ile bahasha. Kwani alijua wazi kuwa kutoka kwake angeweza kupata pa kuanzia. Moyoni mwake hasa alikuwa akimtaka Carlos, hakukuwa na njia nyingine. Kama Carlos aliikosa bahasha yake lazima angemwandama huyo msichana. Hisia zake hazikuwa mbali na ukweli. Hayo yote aliyawaza huku akiagiza Coke na kuichanganya na Konyagi ndogo na kuinywa mfululizo.

"Yes!" akasema mara tu alipomwona yule mwanadada akivuka barabara na kuja upande uleule ambao yeye alikuwepo. Akampa mgongo, naye akapita na kuingia katika uchochoro mmoja uliotenganisha duka hilo na nyumba nyingine. Wakati Amata akijitoa pale katika lile duka, mwanamke mmoja kibonge mfupi alimpita haraka akaingia katika uchochoro uleule. Amata akatulia. Hisia zake zikamtuma kusubiri zaidi. Akafanya hivyo na baada ya watu kama wawili watatu hivi kupita akaingia kijana mmoja aliyevalia jinzi na fulani ya kubana. Shingoni mwake alining'iniza mkufu wa gharama. Amata naye akaingia katika uchochoro huo na kufuata taratibu huku akihakikisha ameona ni kona gani ambayo yule mwanadada ameingilia.

❦

Kwa mwendo wa haraka lakini wenye tofauti kama ya dakika moja katikati, yule mwanamke kibonge aliingia kwenye nyumba moja ambayo alimwona yule mlengwa wake akipotelea humo. Hakuwa na haja ya kuuliza, alikwea ngazi na kujitoma ndani huku akiona mlango gani ulikuwa ukifungwa kwa wakati huo.

'Ngo! Ngo! Ngo!'Aakaugonga na kusubiri nje kwa nukta kadhaa.

"Nani tena, kufika tu ah!" akajisemea yule mwanadada kule ndani na kisha akaufungua mlango kidogo. Aliyemwona hakumjua. Akamtazama juu mpaka chini na yule mwanamke akajisokomeza ndani ya chumba hicho.

"Dada vipi mbona waingia tu hata sijakukaribisha?" akamuuliza.

"Haina haja, ningekuwa mwanaume sawa, lakini mimi ni mwanamke mwenzio hatudhuriani!" akajibiwa.

"Swala sio kudhuriana, hiki ni chumba cha mtu…"

"Sawa vaa blauzi yako kama mwanzo nina shida na wewe," yule bonge akasema.

"Shida!" akashangaa, "kwani we ni nani?" akaongeza swali.

"Mimi ndiye yule mwenye mzigo uliompa mtu usiye wake," akaongeza kusema yule bonge.

"Mzigo!"

"Ndiyo kule kazini kwako," yule mwanadada akabaki kapigwa bumbuwazi na nukta hiyohiyo pale mlangoni akaibuka Carlos, alipogeuka wakakutana macho kwa macho.

"Tunaondoka na wewe mpaka tutakapopata mzigo wetu!" Carlos akazungumza. Yule mwanadada hakuwa na la kufanya alipogeuka kwa yule bonge akakutana na bastola. Macho yakamuwiva kwa kilio, midomo ikamtetemeka kwa hofu. Hakuwahi kuona bastola waziwazi zaidi ya kwenye filam au zile za kuchezea watoto.

"Ukilia tu… nakumaliza," yule mwanamke mnene akaunguruma huku mkono mmoja ukimpa blauzi yake ambayo alikuwa keishaivua na kuitupia juu ya kitanda, "vaa!" akamwambia. Ilichukua sekunde kama hamsini na moja kukamilisha zoezi hilo.

❦

Kamanda Amata alitembea kwa hatua za kawaida na alipoikaribia ile nyumba kulikuwa na watu wengi wengi pale nje. Hali ile hakuifurahia kwani hakupenda kabisa polisi waje kusema 'ulikuwa wa mwisho kuingia, kwa hiyo ndiyo mtuhumiwa namba moja'. Hilo hakulitaka. Lakini alijua wazi kuwa anapoteza muda. Kutoka pale alipokuwa akisubiri alijikuta akizungukazunguka kama aliyebanwa na haja ndogo. Lile kundi lilipoondoka akavuta hatua na kuisogelea ile nyumba, akakanyaga ngazi moja moja na kusimama karibu na mlango wa kuingilia ndani ambao ulikuwa wazi kabisa.

***Itaendelea...***

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani muda wowote kutoka sasa.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (12)

Waote wawili wakaanza safari. Mwizi alimshika mkono Mustafa ili aweze kumuongoza vizuri njiani.

Baada ya muda mfupi, Mustafa akasimama na kusikilizia harufu. “Nyama ya kuku!” alisema. “Kuna mtu anapika nyama ya kuku kwaajili ya chakula cha jioni. Inanukia vizuri sana, hii nyumba wanapenda sana nyama ya kuku jioni, sasa nina uhakika hii ni njia yenyewe.”

Dakika chache baadaye, Mustafa akasema, “nasikia sauti za punda maeneo fulani kushotoni kwetu, hiyo ndio njia inatakiwa tuifuate.”

Dakika chache baadaye, alisimama na kusema,”hiyo sauti ninayoisikia ni ya mtoto analia, hako katoto kila siku jioni lazima kalie tu, labda hakataki kwenda kulala mapema, nafikiri hiyo ndio njia yenyewe huko na nafikiri tunakaribia kufika mahala husika sasa.”

Waliendelea na safari kidogo tena, Mustafa akasimama na kuvuta harufu na kusema, “nakumbuka hii harufu ni ya maua mazuri sana ambayo napenda sana, hii harufu niliwahi kuisikia sehemu moja tu ambayo ndio ile nyumba tunayoitafuta. Nafikiri hapa ndipo mahala tunapohitaji rafiki yangu. Hii ndio nyumba yenyewe, hii ndio nyumba ambayo nilikuja kushona suti ya yule marehemu tuliyekuwa tukimzungumzia.”

Harufu ile ya maua mazuri ilikuwa ikitokea kwenye dirisha zuri la nyumba ya Kassim. Mustafa ameweza kumuongoza mwizi mpaka pale kwenye ile nyumba.

“Una uhakika kwamba hii ndio nyumba yenyewe?” mwizi aliuliza.

“Ndio kabisaaaa nina uhakika kabisa hapa ndipo penyewe.” Mustafa alijibu. “Ila tu siufahamu huu mtaa hivyo hata nyumba yenyewe siwezi kuijua ni ya nani.”

“Hiyo haijalishi. Umenielekeza vya kutosha” alisema mwizi. “umekuwa na msaada mkubwa sana kwangu. Sasa chukua hii sarafu nyingine tena ya dhahabu na nitakuongoza urudi kwenye kibanda chako cha kushonea nguo.

Mwizi akatoa kipande cha chaki kutoka mfukoni kwake na kuweka alama kwenye mlango wa nje wa nyumba ile.

“Hapa sasa nimeshamaliza kazi” alijisemea mwizi. “Nimeweka alama hii mlangoni ili iwe rahisi kwangu kuja. Kwa maana nyumba zote mtaa huu zinafanana, hivyo haitakuwa rahisi kukumbuka. Hii alama ya chaki mlangoni ndio itanikumbusha nitakapokuja kwa mara ya pili. Hapo tutaweza kuvamia na mapanga yetu na kumuua huyu mwizi wa pili wa hazina zetu kule pangoni”

Mwizi akamchukua Mustafa na kumrudisha kibandani kwake kisha akaanza safari ya kurudi msituni kuungana na wezi wenzake. “kiongozi wangu atafurahi sana kwa kazi yangu!” alijisemea huku akicheka. Alipokuwa njiani juu ya farasi wake akawa anawaza jinsi wenzake watakavyokuwa na furaha kupata habari njema ile.

Asubuhi iliyofuata, yule msichana wa kazi Marjane alianza kuandaa chai ya asubuhi kwaajili ya Alibaba na familia nzima. Alichukua birika yenye kahawa na kuandaa machungwa pamoja na sahani na vikombe. Lakini akagundua kwamba hakuna mkate jikoni.

“Itabidi tu nikanunue mkate haraka” alijisemea huku akichukua mfuko na kuelekea madukani hapo mjini. Alipokuwa akirudi, wakati anakaribia mlangoni, akaona alama nyeupe asiyoielewa, akasogea kwa karibu zaidi na kuitazama, ni alama ya chaki imechorwa mlangoni.

“Hii alama haikuwako hapa jana!” alijisemea. “Nani atakuwa ameweka alama hii hapa mlangoni? Na itakuwa ina maana gani hii alama?” Marjane alisimama pale muda kidogo huku akitafakari na kukuna kidevu chake kama mtu anayetafuta ufumbuzi wa jambo fulani.

“Simjui nani aliyeweka hii alama hapa.” Alisema. “sijui pia aliyeweka alikuwa ana maana gani- lakini nafikiri hii alama itakuwa si alama nzuri kabisa. Najua nini cha kufanya.” Akaingia ndani na kuchukua kipande cha chaki. Kisha akatoka nje na kuzunguka mtaa mzima na kuweka alama kama ile mlangoni katika kila mlango wa nyumba zote za mtaani pale.

“Hii lazima itamchanganya huyu anayetaka kufanya ubaya katika nyumba yetu.” Alijisemea huku akitabasamu. Kisha akarudi ndani kumalizia kuandaa chai. Hakumwambia yeyote kuhusu ile alama ya chaki.

**Na. Mwandishi wetu**

SOTE twajua kwamba kila mwaka tarehe 16 ya mwezi Juni ni maazimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika. Hii ni siku iliyobeba historia kubwa sana ya dhuluma ya haki na uhai kwa mamia ya watoto huko Soweto, Afrika ya Kusini.

Mataifa mbalimbali ya Afrika yameadhimisha siku hii kwa namna tofauti tofauti. Hata hapa kwetu Tanzania sehemu mbalimbali zimeadhimisha siku hii.

Kwa namna ya pekee katika Jiji la Dar es salaam, husan Wilaya ya Kinondoni, Mtoto wa Afrika iliazimishwa kwa namna yake ikijumuisha watoto mbalimbali kutoka katika viunga na vitongoji vya wilaya hiyo na kukutana pale Manzese Argentina.

Kaulimbiu ya siku hiyo ilikuwa Elimu Jumuishi Izingatie Ubunifu na Maadili. Ratiba ya siku hiyo iliongozwa na watoto wenyewe. Miongoni mwa wageni walikuwamo viongozi wa serikali; Meya wa Kinondoni, wadau wa maendeleo na wazazi.

Nyimbo, ngoma, mashsiri na maigizo vilikuwa ni sehemu ya burudani kwa waalikwa. Risala iliyobeba ujumbe mufti na mzito iliwasilishwa.

Asilimia kubwa ya watoto walioshiriki ilikuwa ni kutoja shule za Tandale, Manzese na Madale—watoto yatima na waishio katika kaya masikini za maeneo hayo. Mafanikio ya tukio hili adhimu yalichagizwa na Anna Mbise Mobile Library ambao waligawa vitabu bure kwa washiriki ikiwa ni moja ya uhamasishaji wa usomaji vitabu.

Pamoja na wadau wengine kama ATD Tanzania, Tungo Tata TV na marafiki wengine waliweza kuifanisha siku hii.

Anna Mbise, Mkurugenzi wa Anna Mbise Mobile Library anasema, “Pamoja na shughuli zangu za uhamasishaji wa usomai na uandishi wa vitabu kwa rika zote, nimekuwa pia nikiratibu mtandao wa watoto waandishi na wanaharakati wa Afrika. Mtandao huo unaitwa Pan-Africa Young Writers and Activists (PAYWA)..”

Hapa anatuburudisha na shairi murua

Afrika iliyo bora,
Watoto ndiyo vinara,
Wapewe malezi bora,
Elimu yenye ubora,
Watakwepa ufukara,
Wataendeleza bara,
Maarifa ni mtaji.

Ngurumo ya Mwandishi tunampongeza sana Bi. Anna Mbise kwa harakati zake hizi na tunawaomba wadau na marafiki wa elimu kote nchini kuunga mkono kwa namna moja au nyingine wale wote wenye nia ya dhati ya kumkomboa Mtoto wa Afrika.

## Elimu Jumuishi Izingatie Ubinifu na Maadili




Anna Mbise akionesha moja ya furaha zake katika tukio la Mtoto wa Afrika pale Manzese Argentina.

# SHUBAKA LA VITABU

Katika safu ya SHUBAKA LA VITABU toleo hili la 32, tumembamba Fadhy Mtanga akiwa anapekuapekua kwenye shubaka lake. Na katika upekuzi wake huo anakutana na chambuzi bora sana iliyofanywa na mwandishi mufti kabisa Joseph Shaluwa. Chambuzi hiyo ilikuwa ni juu ya kitabu chake (Fadhy) chenye anwani RAFU. Kwanini Rafu? Hebu tusiklize...

***Inaendelea kutoka toleo lililopita…***

1. LUGHA
Mwandishi na mtunzi wa riwaya hii Fadhy ameonyesha umwamba wa kujidai na lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kiasi katika namna ya kuvutia sana na isiyochosha.

2. WAHUSIKA
Fadhy ameonyesha utundu mkubwa katika kuwajenga wahusika wake. Kila mmoja na tabia zake. Kila mmoja na maneno anayopenda kutumia.

3. KOZI YA BURE YA KIINGEREZA
Fadhy ameonyesha alivyo mwelewa wa lugha ya Kiingereza, lakini akitumia ufundi wake kufafanua kwa Kiswahili chepesi mbele ya maandishi mengi aliyolazimika kuyatumia kwa Kiingereza.

4. MAJIGAMBO
Ndani ya RAFU, wahusika wake wamejaa majigambo. Kuna ufundi wa lugha umetumika, hasa kwenye mazungumzo.

5. TAALUMA
Mtunzi anaonekana kuandika kitabu hiki kwa muda mrefu. Kwa uzoefu si chini ya miezi mitatu. Lakini inaonyesha huenda alifanya tafiti kwa muda si chini ya mwaka mmoja kujua kwa kina kila eneo alilokusudia kuliandika.

6. MANDHARI
Nina hakika mwandishi anapenda kusafiri sana, ama alisafiri kwa lengo la kuijua miji yote aliyotaka kuiweka kitabuni. Ama alitafiti kwa kutumia mtandao au watu wa karibu walioishi katika maeneo aliyotaka kuyaandika.

7. STAILI YA UANDISHI
Kwanza kutumia nafsi ya kwanza — umoja. Ni staili ngumu sana na inamnyima mwandishi uhuru. Ili uimudu staili hii lazima uwe na utajiri wa maneno, ambao Fadhy anao.

8. ANAFANANA NA NANI?
Kila mwandishi huwa na waandishi waliomtangulia anaowahusudu ambao pengine huiga staili zao. Mwandishi mahiri, anaweza kumhusudu mwandishi fulani, lakini asimuige, jambo ambalo ni gumu sana.

9. KAVA
Kava ni bora sana. Simple. Linajieleza. Linaeleweka. Linapendeza. Unaweza kulichukulia poa, lakini naamini designer alitumia muda mwingi sana kwenye utayarishaji wa kava hilo.

10. UHARIRI
Mhariri amefanya kazi kubwa sana. Ni kitabu cha kurasa 254, chenye kadirio la maneno kama 65,000–70,000 hivi. Lakini hakuna makosa ya lugha kabisa. Lugha imenyooka sawasawa.
MWISHO

Katika kipindi cha mwaka mmoja, RAFU kinakuwa kitabu changu namba moja kwa ubora wa jumla kati ya vitabu nilivyosoma katika kipindi hicho.

***MCHAMBUZI: JOSEPH SHALUWA***
***APRILI 2, 2020,***
***KWEMBE — UBUNGO,***



# KITABU NILICHOSOMA

## CORE GENIUS

**ANNA MBISE MOBILE LIBRARY**

**KITABU**: Core Genius -Jinsi ya kugundua uwezo wako wa kipekee
**MWANDISHI**: Joel Nanauka
**MSOMAJI**: Isack Akyoo
**TOKA** :Zanzibar

Niliyojifunza toka Kitabu hiki

Utangulizi,
Kitabu hiki cha *Core Genius*- Jinsi ya kugundua uwezo wako wa kipekee kimewezesha kufunua mambo ambayo shuleni hayafundishwi. Hivyo ni kitabu muhimu kwa kumsaidia mtu kujijua uwezo wake ambao hajawahi kuuonyesha toka azaliwe kama ifuatavyo.

1. Kila mtu ni core Genius kwenye eneo lake la maisha
Albert Einstein aliwahi kusema kuwa "Kila mtu ni Genius.Lakini kama utamhukumu samaki kwa kushindwa kupanda juu ya mti, basi samaki ataishi maisha yake yote akiamini kwamba hana akili" (*Everyone is a genius but if you judge a fish by its ability to climb a tree, it will live its whole life believing that it is stupid).*

Hivyo hakuna mtu ambaye hana uwezo wa kufikia kilele cha mafanikio yake. Hii inamaanisha kama ameshindwa hili unaweza lile.

Moja kati ya fumbo kubwa lililojificha katika safari ya mafanikio ya mwanadamu ni kujua uwezo wake wa kipekee .

**Maana ya CORE GENIUS**
Core Genius ni NGUVU YA KIPEKEE aliyonayo mtu ndani yake. Hii nguvu ukiitumia vizuri humfanya mtu kuwa wa tofauti kwa mfano umefeli darasani lakini ukagundua unakipaji cha kucheza mpira, kuimba muziki, kukimbia riadha hiyo sasa ndiyo nguvu ya kipekee ambayo haipimwi darasani.

Hapa kuna tafsiri kuu tatu za kumtafsiri mtu mwenye uwezo wa kipekee

i) Kile kitu kinachokutofautisha kirahisi *(key differenter)*
Hapa kwetu Tanzania tumchukue Diamond kama mfano wetu, hajasoma sana lakini ile NGUVU YA KIPEKEE aliyonayo imemfanya amejitofautisha na wanamziki wengine. Tumwangalie Aishi Manula mchezaji mpira kawa Tanzania one kwasababu ya uwezo wake wa kipekee.
Hivyo kinachokutofautisha na wengne ni NGUVU YA KIPEKEE.

ii) Ni kile kitu kinachokufanya MKAMILIFU
Yaani ukitaka kufanya jambo lako unamuwaza kaka au dada fulani atafanya kikamilifu tofauti na wengine yaani hata usipokuwepo mambo yanakuwa safi. Unataka kujenga, kushona nguo, kuendeshwa kama una gari basi unajua nikimpata fulani inapendeza

iii) Kuangalia ujuzi, maarifa na uzoefu wako
*(The combination of knowledge, skills, experience and traits )*

Mambo 3 ya kukuongoza katika tafakari yako:-
i) Mambo uayoyapenda*(passion)*
ii) Kitu unachokiweza, una ujuzi na uzoefu nacho
iii) Watu wako tayari kukulipa

**Kuishi kwenye Core Genius yako, maana yake nini?** Ni pale ambapo, unafanya UNACHOKIPENDA na ambacho una UWEZO nacho wa kukifanya, na wakati huo huo watu wako tayari KUKULIPA kwa unachokifanya.

**2. Aina za core Genius na namna ya kuzigundua**
Kwa miaka mingi wataalam wa UBONGO waliamini kuna aina tatu za kujifunza
i) Kuona
ii)Kusikia
iii)Vitendo
Lakini mwaka 1983 Dr. Howard Gardner aligundua kuna aina nane kupitia kitabu chake
cha "Frames Of Minds" (Theory of Multiple Intelligencies ).

Katika utafiti wake aligundua aina nane za uwezo wa kipekee ambazo wanadamu wanazo na kuwa mfumo wa shule umejikita katika kufundisha aina mbili tu. Hii imesababisha watu wengi sana wafeli kwenye maisha hasa baada ya kufeli shule kwa sababu waliamini kuwa hawawezi kufanikiwa tena.

Katika kutathimini uwezo wa kipekee kuna mambo matatu muhimu kuyazingatia
1. Watu wako tofauti kulingana na walivyo, hakuna mtu anayefanana na mwingine duniani kiuwezo wa kipekee *(core Genius)*
2. Hatufanani namna ya kuchakata taarifa
3. Elimu yeyote unayoipata ina maana sana kama utaitumia vizuri

***Itaendelea toleo lijalo***



FROMA
Liquid Detergent







- **Tunauza Multipurpose Soap jumla na rejareja.**
  **Lita 3 kwa Tsh 3,000**
  **Lita 5 kwa Tsh 10,000**

- **Tunauza mitandio ya kisasa kwa akinadada na akinamama wa kileo Tsh 10,000**

- **Tunauza mataulo mazuri sana, kwa rika zote Tsh 15,000**

**Tunapatikana**
**Dar es salaam**
**KIMARA BARUTI.**
**Mikoani tunatuma.**

**Mawasiliano:**
**Simu: 0654899743**
**Instagram: froma1326**

**Karibu tukuhudumie!**





TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## TUWAPENDE TUWALINDE

Afrika ni bara letu, tukufu lilotukuka
Hapa ni nyumbani kwetu, sote ni dada na kaka
Kila kilichomo chetu, hakuna mwenye kuzuka
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika.

Tamaduni za kileo, zatupaisha upepo
Malezi ni ya kileo, kizazi chenda upepo
Twahangaikia leo, twasahau kesho pepo
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika

Ukatili kwa watoto, mekuwa sugu hakika
Wazazi mioyo joto, watoto shule kufika
Twabaki mpotopoto, na kumwachia Rabuka
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika


Mahakama twazitaka, kusimamia sheria
Rushwa iwe takataka, watoto kupigania
Kataeni katakata, hongo ikikufikia
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika

Dunia sasa yatisha, ndugu mekuwa adui
Usiku ukikatisha, watoto hawatambui
Wawabaka vya kutisha, eti hatuwatambui
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika

Malezi twawapatia, watimize ndoto zao
Jahili ladhamiria, kukatisha ndoto zao
Sononi mwaachia, ni giza kwa kesho zao
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika

Sote na tuwe walinzi, kwa watoto wote pia
Tuanike mabazazi, wenye hii mbaya tabia
Yawe salama makazi, kwetu na watoto pia
Tuwapende tuwalinde, watoto wetu Afrika.

**Shujaa Maneno**
**Bagamoyo Pwani.**



**HAPPY BIRTHDAY**
**COMRADE JOEL NANAUKA**

Nani mpenda vitabu viletavyo mabadiliko chanya katika jamii hususan katika kujikomboa kiuchumi asiyelijua jina hili?

Yawezekana umesoma sana vitabu vyake vilivyoja-wa 'madini' ya kutosha ya kukufanya kuwa mtu mwingine lakini hujawahi hata kuiona sura yake. Huyu hapa pichani, mwamba wa Mtwara {Tuacheni wa Mtwara tunatisha}

Tarehe 4 Julai, ilikuwa kumbukizi ya mazazi yake. Tumshukuru Mungu kwa zawadi ya maisha yako. Kalamu yako imebadili maisha ya Watanzania wengi. Ngurumo ya Mwandishi tunasema **Happy Birtday to you!**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# Habari Picha



Mariam Mbano, mwandishi wa KOVU LA MOYO akiwa na Tuzo yake ya USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII MSAADA WA KISHERIA NA UCHUMI. Tuzo hiyo alitunukiwa na Taasisi ya Joyful Foundation tarehe 22/6/2024.




**Mtoto Babra alipotembelea meza ya vitabu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Pichani akiwa na Bi. Anna Mbise, Mkurugenzi wa Anna Mbise Mobile Library.**

**Kabila letu ni Vitabu na Lugha yetu ni fasihi. Pichani, Anna Mbise, Mkurugenzi wa Anna Mbise Mobile Library na Richard Mwambe Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Kitabu Maisha walipokutana kwa mbadilishano wa mawazo.**





**Tumlinde mtoto wa Afrika kwa Afrika ya kesho. Picha yenye mguso wa kipekee... 'JISHUSHE'**

# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—2

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

**MSIMULIZI wa hadithi hii ni ndugu Mpepo wa kijiji cha Tetere mkoani Rukwa. Yeye ana umri wa miaka thelathini na tano (wakati huo) na ameoa. Habari za maisha yake kwa ujumla zinajitokeza ndani ya hadithi yenyewe. Ili masimulizi yake yasiathirike, hebu tumsikilize yeye mwenyewe anatuambia nini katika sura hii ya kwanza.**

**SURA YA KWANZA**
**Uamuzi wa watu wazima**

*Inaendelea...*

Baada ya muda kidogo nilijikuta naloa kifua changu. Machozi yalipita kwa wingi upande wa kushoto na kulia wa pua yangu ambayo nayo ilianza kutoa kamasi nyepesi. Machozi yalikuwa mengi. Mengine yalibidi yaifunike pua kwa muda. Yalikwenda kama mawimbi yasiyo na haraka. Jambo ambalo nilikuwa silielewi.

Mara nilisikia mtu akibisha hodi. Kule kusikia sauti yake nikafahamu kuwa alikuwa Luzolo, rafiki yangu mkubwa. Lengo lake hasa lilikuwa kuja kunituliza kuhusu mkasa ule. Usemi kwamba 'Rafiki mzuri ni yule akujuaye katika dhiki,' ulidhihirika. Wakati ule mimi na mke wangu tulikuwa katika machungu makubwa baada ya tendo langu la kupigana. Hata hivyo lingeweza kuitwa tendo la aibu kama ningemkimbia Selemani. Pengine angelinishinda mbio na kuanzisha vita kama vile. Kwa haya, Sofi mke wangu aligeuka na kujifuta machozi akatulia. Lakini ilimchukua muda kabla ya kuanza kumwangalia Luzolo. Uso wake ulionesha kuchoka. Uchovu wake ulikuwa na sababu.

Luzolo naye alikuwa mtu mtambuzi sana. Alielewa ni nini kilichokuwa katika nyumba yetu. Mtu akiwa na akili tambuzi hakika ndiye mwenye busara. Kwa heshima yake alifanikiwa kuibadili hali ya huzuni kuwa furaha isiyopimika. Alielezea vituko mbalimbali vilivyowahi kumpata yeye. Alianza mikasa ya kunusurika na radi, kuvamiwa na majambazi, kukataliwa na wachumba, kufukuzwa na samba; na mambo mengine mengi. Alipomaliza, nilihisi kuwa mkasa wangu wa siku ile haukustahili kushangaza. Lo! Ajabu gani hiyo? Luzolo, mtu ambaye nilidhani hajawahi kupata taabu yoyote, kumbe yalimfika mambo mengi vile!

Sasa naukumbuka wimbo wa kikundi fulani cha muziki kiitwacho 'Simba wa nyika'. Vijana hao waliimba wimbo usemao 'Vumilia iko siku moja tabu itakwisha'. 'Kumbe yafaa kuvumilia. Lakini kusema taabu itakwisha siku fulani ni namna ya kujituliza. Jambo hili litatoweka muda wa kuishi duniani utapokwisha. Rafiki yangu Luzolo, ambaye ni baba wa watoto wanne ana maisha mazuri na famili yake, hata hivyo matatizo bado hayajamwisha. Tulipofikia hapo tukakubaliana kuwa matatizo ni sehemu ya maisha.

Mke wangu alituchekesha sana alipotukumbusha kwamba mtu akiona ana matatizo afahamu kwamba bado anaishi. Hoja yake ya pili ikawa kuwa ingawa vipengele fulani vya utamaduni hutofautiana katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, matatizo hayakosekani. Hivyo matatizo vilevile ni utamaduni.

Lo! Kumbe mwalimu wangu aliyeniambia utamaduni ni ngoma na nyimbo za kiasili hakukamilisha. Luzolo akasema utamaduni ni mtindo wa maisha ya watu au jamii fulani. Hivyo unahusu pia dini, nyimbo, michezo, lugha, ndoa, miiko na itikadi nyingine.

Anna, shemeji yangu akaandaa kahawa na kutuandalia wakati tukiendelea na mazungumzo yetu. Kila mmoja wetu akaanza kunywa kinywaji. Anna na mama Tabu waliweka asali katika vikombe vyao. Luzolo yeye alitaka kahawa tupu bila asali. Basi mimi nilipoona hivyo name nikajidai pia nataka kama yeye. Hayo hayakuwa matakwa yangu. Ilitokana na kumwona Luzolo mwenzangu akifanya vile kinyume na kina mama walivyopenda. Nikawa mtumwa wa mawazo. Hata hivyo, nilikifurahia kinywaji changu. Moyoni nikawa nawaza kuwa iwapo ingekuwa vile kila siku ingalikuwaje? Gharama ya kununua makopo ya asali kila mwezi ingelikoma.

***Itaendelea toleo lijalo...***

# ELIMU JAMII

## Ukamataji, Upekuzi na Dhamana ya Polisi—4

### UPEKUZI WA KUIDHINISHA UPEKUZI

**Mamlaka zifuatazo zimepewa mamlaka na uwezo wa kuidhinisha upekuzi:**

1. Mkuu wa kituo cha polisi
2. Hakimu

### UWEZO WA MKUU WA KITUO CHA POLISI KATIKA UPEKUZI

**Kifungu cha 38** cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinampa uwezo na mamlaka afisa wa Polisi ambaye ni mkuu wa kituo cha polisi (OCS) anapokuwa amepokea taarifa za kuaminika kwamba ndani ya nyumba, jengo au eneo fulani au kwenye chombo cha usafiri kuna:-

a) Kitu au vitu visivyo halali kama vile bangi, gongo, dawa, silaha, nyara n.k

b) Kitu au vitu ambavyo vimetumika kutendea kosa la jinai kama vile kisu, bunduki, sumu n.k

c) Kitu au vitu ambavyo kwa sababu ya msingi vinasadikiwa kutumika kutendea kosa la jinai, kama vile bunduki na kwamba mkuu huyo wa kituo anaamini kwamba ucheleweshaji wowote wa kufanyika upekuzi, unaweza kusababisha utoroshwaji au uharibifu wa kitu au vitu vinavyotafutwa au vinaweza kuhatarisha maisha ya binadamu au mali. Mkuu wa kituo anao uwezo wa kutoa amri ya upekuzi kufanyika haraka. Amri ya upekuzi haitolewi kwa mdomo, ila kwa maandishi na hati maalum ya Polisi ijulikanayo kama *Amri ya Upekuzi* au kwa Kiingereza **'Search Order'.**

### UWEZO WA HAKIMU KATIKA SUALA LA UPEKUZI

Hakimu anao uwezo na mamlaka ya kuamuru upekuzi ufanyike kwenye nyumba, jengo au eneo lolote baada ya kupokea malalamiko au taarifa za kuaminika kwamba kwenye nyumba, jengo au eneo fulani kuna kitu au vitu vizivyo halali au vielelezo muhimu. Amri hii hutolewa kwa maandishi na hujulikana kama ***Hati ya Upekuzi*** kwa Kiingereza ni ***Search Warrant.***

### UWEZO WA KUPEKUA KWENYE VYOMBO VYA USAFIRI

**Kifungu chs 25** cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai kinampa mamlaka na uwezo afisa wa polisi ***kusimamisha, kuzuia na kupekua*** chombo chochote cha usafiri anapokuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa ndani ya chombo kuna:

a) Mali au kitu chochote kisicho halali kama vile mali ya wizi, magendo, silaha, dawa za kulevya, nyara n.k

b) Kitu au vitu vyovyote vile vinavyoweza kutumika kutenda kosa la jinai kama vile silaha, sumu n.k

c) Watu au mtu yeyote ambaye anamshuku au anazo taarifa za kuaminika kuwa mtu huyo anatafutwa na Polisi au mahakama, au watu au mtu huyo anahusiana na vitu vilivyoorodheshwa kwenye kifungu (a) na (b) hapo juu.

### UWEZO WA KUVUNJA, KUINGIA NA KUFANYA UPEKUZI

Kifungu cha 43 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinampa uwezo afisa wa Polisi kuvunja na kuingia kwenye nyumba au jengo au

mahali popote kwa madhumuni ya kufanya upekuzi, iwapo patakuwa pamefungwa na mmiliki anakataa kutioa idhini baada ya kuoneshwa hati ya kuamuru upekuzi ufanyike.

## UPEKUZI WA DHARULA

**Kifungu cha 42** cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinampa uwezo afisa wa Polisi kufanya upekuzi wa dharula kwenye nyumba, jengo au mahali popote endapo anazo sababu za msingi za kutaka kufanya upekuzi wa dharura. Upekuzi wa dharura hufanyika bila hati ya kuidhinisha upekuzi yaani **search order** au **search warrant**. Upekuzi huu hufanyika baada ya mzingira kulazimu uharaka na kwamba kutokufanya hivyo kutasababisha uharibifu, au utoroshwaji wa kitu au vitu au mtu anayetafutwa kuhusiana na shaka au tuhuma.

## MUDA WA KUFANYA UPEKUZI

sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai haitamki saa za kufanya upekuzi, ila inasema upekuzi utafanyika kuanzia mawio hadi machweo ya jua. Pia ni muhimu ieleweke kwamba, chini ya kifungu cha 42 upekuzi unaweza kufanyika hata usiku.

***Katika toleo lijalo tutaangazia Dhamana ya Polisi. Usikose na waweza kutupa maoni yako kupitia WhatsApp 0766974865***

## SAIKOLOJIA: ITUNZE NGUVU YAKO YA ASILI

***Inatoka ukurasa wa 7…***

**b} Jiamshe upya**

Saikolojia ya akili yako ikikuthibitishia kuwa uwezo wako umepungua basi haraka sana jiamshe upya wewe mwenyewe. Hii inaweza kuwa tiba nzuri sana ukijifanyia. Kwanza tafakari ni wapi au ni kwa sababu zipi za pale juu nilizoziainiasha zimekupelekea kupunguza au kulaza uwezo wako wa asili. Ukishazijua sababu basi anza kuzipangua sababu zote. Jiamshe wewe mwenyewe, jiongeleshe, jisemeshe kwamba wewe ni nani? unataka nini? kwanini umelaza uwezo wako wa asili? Yote hayo yafanyie mahali ukiwa peke yako pengine ikiwa chumbani kwako.

**c} Ruhusu maoni ya uwaaminio.**

Karibisha maoni ya baadhi ya watu unaowaamini. Kuna watu wanaokupenda ambao hawatopenda kuona ukipotea, ruhusu kuwasikiliza.

Baada ya kufanya yote hayo hapo juu basi jitahidi kuitunza nguvu yako ya asili, utaitunzaje? kwa kuyafanya yale ambayo yataulinda uasili wako, jiepushe kufanya yale yatakayoipoteza asili yako, yale yote niliyoyaonesha hapo juu kuwa yanaweza kuwa sababu ya kuuua uasili wako. Mungu atutangulie sote.

Karibu kwa mashauriano ya maisha, nafanya shughuli zangu popote pale ninapotakiwa kufanya kwa makubaliano na bei tutakayoelewana. Iwe ni masuluhisho ya ndoa, mahusiano, ama hata mitihani ya maisha pia. Nguvu yangu ya asili inaniwezesha kuyamudu mambo yangu na ya wengine pia, karibu sana ikiwa unahitaji huduma ya ushauri, nafanya kazi kwa njia zozote. Iwe kwa simu au ana kwa ana (kwa mtu au watu kugharamia nauli, malazi na chakula na posho pia ya kazi). Karibu sana. Nikuhakikishie hautojutia kunipa kazi ya maongezi nawe. Kwa pamoja tuyafanye maisha kuwa na thamani.

Kwa ndugu zangu Kenya, nawapenda sana, na nawaombea kwa Mungu mvuke hapo. Mungu awalinde.

Ndugu zangu Tanzania, Mungu atulinde daima. Nawapenda.

Asante, nikutakie majukumu mema.

**The Magic Author.**

**Madame Neema Mgao.**

**Tangazo**




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com